HOTUBA YA MHESHIMIWA BAHAME TOM NYANDUGA, MWENYEKITI WA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA KATIKA SIKU YA KUPINGA MATESO NA UKATILI DHIDI YA WAZEE DUNIANI, TAREHE 15/06/2017, YALIYOFANYIKA KATIKA OFISI ZA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA, JENGO LA HAKI, DAR ES SALAAM.

Mh. Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,

Waheshimiwa Makamishna wa Tume.

Mkurugenzi Mkuu , HelpAge International Tanzania,

Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,

Waheshimiwa wawakilishi wa Balozi za nchi mbalimbali mliofika,

Ndugu wawakilishi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa,

Ndugu zangu Viongozi wa Mashirika yasiyosimamia haki za wazee,

Ndugu Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii,

Wawakilishi wa Idara za Serikali, mashirika ya kiserikali na Azaki,

Viongozi wa madhehebu ya dini,

Wazee wote mlioko hapa,

Ndugu wanahabari,

Mabibi na Mabwana,

Aslaam Aleykum, habari za asubuhi.

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima wa kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa salama. Napenda kuwakaribisha hapa makao makuu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Pili napenda nitumie fursa hii kuwashukuru ndugu zetu wa HelpAge International Tanzania kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kuandaa mkutano huu. Mimi binafsi nawashukuru kwa heshima kubwa

mliyonipa ya kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya siku ya kupinga mateso na ukatili dhidi ya wazee Duniani. Pia nashukuru kwa niaba ya Tume ushirikiano uliopo kati ya Tume na taasisi zinazosimamia haki za wazee. Hii ni mara ya tatu Tume kufanya mikutano inayohusu haki za wazee. Awali tulifanya kongamano la haki za wazee mwezi Juni 2015, halafu Tume iliitisha mkutano tarehe 21Oktoba 2015 siku ya haki za Binadamu Afrika na tukazungumzia haki za wazee. Tume pia imeshiriki mikutano kadhaa iliyoandaliwa na taasisi za wazee huko Magu, Kibaha na Dar Es Salaam.

Napenda pia nitambue na nishukuru ushirika wa serikali-Idara ya Ustawi, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, katika mkutano huu.

Nichukue muda mfupi kuitambulisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kwa wale wasioijua. THBUB ni chombo cha kitaifa kinachofanya kazi pande zote za Muungano ili kuhamasisha, kulinda, na kutetea haki za Binadamu kama zilivyoainishwa ndani ya Katiba ya nchi ya mwaka 1977, na mikataba wa haki za Binadamu ya Afrika na Umoja wa Mataifa ambayo Tanzania imeridhia. Tume hii ilianzishwa mwaka 2001. Napenda niwashukuru wajumbe waliotoka Zanzibar na mikoa yote, mliopo hapa.

'HelpAge International" ni shirika la Kimataifa, lililofungua ofisi yake Tanzania mwaka 1993. Malengo yake makuu ni:

i) Kukuza ustawi wa wazee wanawake na wanaume,

ii) Kuhakikisha kipato cha wazee kinapatikana,

iii) Kuondoa ubaguzi dhidi wazee.

Ndugu wageni waalikwa, siku hii ya leo inatukumbusha umuhimu wa kuwatetea wazee ili wawe na maisha bora na yenye matumaini wakati wanapostaafu au wanapokuwa na umri mkubwa. Katibu ametukumbusha maudhui na malengo ya siku hii ya leo.

Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambua **haki ya kuishi,** inasema " *Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria*". Ibara ya 16 ya Katiba, inatambua haki ya ulinzi wa nafsi yake (Physical integrity). Pamoja na

kwamba haki ya kuishi ya wazee na ulinzi wa nafsi yake zinatambulika, bado suala la hifadhi ya maisha ya wazee inakumbana na changamoto nyingi.

Wazee wengi wamekuwa hawathaminiwi baada ya kulitumikia taifa kwa muda mrefu katika utumishi wa serikali au katika jamii. Ni wajibu wa jamii kuwathamini na kuwalinda wazee. Ukatili wanaofanyiwa wazee hapa Tanzania na duniani kote ni pamoja na kuwanyanyapaa, kuwauwa kwa tuhuma za ushirikina, kupigwa, kutukanwa, n.k. Mambo ambayo Tume inayalaani. Hapa Tanzania takwimu za Jeshi la polisi zinaonyesha kuwa jumla ya wazee 245 waliuawa kwa imani za kishirikina katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2014 ambapo kati ya hao wanaume walikuwa 16 na wanawake 229. Mauaji hayo yalitokea katika mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga, na Tabora, Simiyu na Geita.

Wazee ni kundi muhimu, katika jamii linalohitaji ulinzi na utetezi wa haki yao kwa kuwa katika umri huu wanakuwa wanyonge kutokana na umri mkubwa, hali zao za kiuchumi, matatizo ya kiafya ambayo husababisha matatizo ya kisaikolojia na sonono (depression).

Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, inaonyesha kuwa idadi ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka sitini Tanzania ni 2,507,568, kati ya hao wanawake ni 1,307,358 na wanaume ni 1,200,210. Kwa mujibu wa Sensa hiyo, Wazee ni asilimia 5.6 ya Watanzania wote 44,928,923, ambapo asilimia 80 ya wazee hao wanaishi vijijini, na wanatunza asilimia 50 ya yatima wote nchini.

Sera ya wazee ya mwaka 2003 imetoa miongozo katika kupanga, kutekeleza, na kutathmini utoaji wa huduma kwa wazee. Malengo makuu ya sera ni kuhakikisha kuwa wazee wanatambuliwa,wanapewa huduma za msingi za jamii na kupewa fursa katika kushiriki shughuli za kila siku za jamii. Sera ya wazee inawajibisha serikali kuhakikisha kuwa:

- Wazee wenye umri usiopungua miaka 60 wanapata huduma za afya bila malipo na wasichangie gharama,
- Inaandaa utaratibu wa kufuatilia afya ya wazee,
- Inaandaa utaratibu wa kupanua uelewa wa wazee kuhusu maambukizi ya VVU na mafunzo ya wahanga wake,

- Wazee na umma kwa ujumla wafahamishwe kuhusu matatizo ya afya ya wazee.

Zipo jitihada za makusudi ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kuhifadhi haki za wazee zikiwemo za kukomesha ukatili kwa wazee katika jamii, hususani kuchukua hatua dhidi ya mauaji yaliyokuwa yanafanyika kanda ya ziwa. Kwa mfano wilaya ya Magu mkoa wa Mwanza, ina mabaraza ya wazee yapatayo 20 kwa ngazi ya kata na mabaraza ya wazee 70 kwa ngazi ya kijiji, ambayo yameundwa kwa mujibu wa taratibu na mwongozo wa sera ya wazee ya mwaka 2003. Kazi za mabaraza haya ni kuwatambua na kuwaunganisha wazee wote ili kuwa na sauti moja katika kutatua matatizo yao na kudai haki zao za msingi. Tume inashauri kwamba serikali ihakikishe mikoa yote inaanzisha mabaraza hayo.

Lakini pamoja na uwepo wa sera ya wazee bado Bunge halijatunga sheria inayoainisha na kulinda haki za wazee.

Zipo hatua mbali mbali ambazo Serikali inazichukua zenye kuleta ahueni kwenye maisha ya mzee hapa nchini kwa mfano mpango wa TASAF wa kusaidia familia zisizo na uwezo. Pamoja na jitihada hizo misaada hii haiwafikii walengwa wote. Kwa upande wa Tanzania Visiwani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshaanza kuwalipa pensheni wazee tangu mwezi Aprili mwaka 2016. Tume inaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (S.M.Z.) kwa hatua ilizochukuwa.

Ndugu washiriki wito wangu leo ni kuomba Serikali kuharakisha mchakato wa kuwaingiza wazee wote katika mfumo wa malipo ya Pensheni na itunge sheria ya kulinda haki za wazee.

Aidha, Serikali imefanya juhudi ya kuanzisha mfuko wa Afya ya jamii (CHF) hasa maeneo ya vijijini ambapo wazee wananufaika. Hili ni jambo la kupongezwa, Ndugu waalikwa. Mkurugenzi wa HelpAge amezungumzia ongezeko la idadi ya wazee duniani Mwaka 1961, “life expectancy” ya Mtanzania ilikuwa ni miaka 45. Miaka ya 1970-1980 hali hii ilitetereka kutokana na janga la ukimwi. Nadhani sasa “life expectancy” ni miaka 62. Kwa hiyo ongezeko hilo linaonyesha kuwa lishe na afya katika taifa zimekuwa bora. Tatizo ni kwamba hatujajipanga vizuri kusimamia uhai wakati wa uzee uliotokana na ubora wa afya na kuishi miaka mingi, katika ngazi za familia, taifa na jamii. Yapo yanayoweza kufanyika kuhusu

sera, yapo ya sheria lakini yapo ya jamii, yaani maswala ya heshima na adabu tu, kwa mfano vijana kuwalinda, kuwatunza na kuwaenzi wazee.

Kwa hiyo basi lengo la mkutano huu, pamoja na kuadhimisha siku ya kupinga ukatili na mateso kwa wazee duniani, pia ni kujadili kwa kina changamoto zinazowakabili wazee pamoja na hatua mbalimbali zinazochukuliwa au zinazopaswa kuchukuliwa na serikali na taasisi zisizo za serikali, katika kuzikabili changamoto hizo.

Kwa ufupi tu changamoto zinazowakabili wazee ni pamoja na:

- Umasikini wa kipato,
- Kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi, hivyo kushindwa kuongeza kipato,
- Magonjwa mengi kutokana na kupungua kwa kinga mwilini,
- Lishe duni,
- Manyanyaso au unyanyapaa,
- Mauaji kwa imani za kishirikina,
- Kutoshirikishwa katika ngazi za maamuzi,
- Ukosefu wa sheria ya ulinzi wa haki ya wazee, pensheni n.k

Hivyo ni muhimu kuzibainisha changamoto hizi na kupendekeza mikakati zaidi ya kukabiliana nazo. Napenda nitoe mrejesho, baada ya Mkutano wa tarehe 21 Oktoba 2015, Tume ilifikisha maazimio ya mkutano ule kwa Mh. Mzee Ali Hassan Mwinyi Rais mstaafu wa awamu ya pili, na Wizara ya Afya kwa ajili ya utekelezaji wake. Tunashukuru kwa ushirikiano wa serikali walioonyesha kwa kaimu Kamishna wa Ustawi wa jamii na watendaji wake na ofisi nyinginezo kuwepo hapa leo.

Hitimisho.

Baada ya kusema haya napenda nitumie fursa hii kuishukuru kamati ya maadhimisho ya siku hii kwa kufanikisha maandalizi na hatimaye kutukusanya katika ukumbi wa Tume leo hii. Maadhimisho haya yanaonyesha jinsi ambavyo

washiriki wote walivyojitoa kutetea haki za wazee.Tutumie siku hii katika kuzielewa changamoto hizi na kuendeleza utetezi na ulinzi wa haki za wazee. Kauli mbiu ya mwaka 2017 inasema "***elewa na kukomesha unyanyasaji wa kipato kwa wazee-haki za binadamu".*** Jukumu hili linaanza sasa**.**

Nawatakia kila la kheri kwa maazimio mtakayokubaliana. Kwa maneno haya machache napenda kutamka mkutano umefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.